

CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI



SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI (CERVIX)



UTANGULIZI

Saratani ya mdomo wa kizazi ni saratani inayoongoza kwa vifo vingi vya wanawake hapa Tanzania. Pamoja na hali hiyo, saratani hii inatibika iwapo ugunduzi utafanyika mapema.

NINI CHANZO CHAKE

Husababishwa na aina ya kirusi kinachoitwa Human Papilloma Virus (HPV). Kirusi hiki huambukizwa kwa njia ya kujamiiana na mtu mwenye maambukizi ya Human Papilloma Virus.

DALILI ZA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI


- Kutokwa na damu baada ya kujamiiana
- Kutokwa na uchafu ukeni
- Kutokwa na majimaji yenye harufu mbaya ukeni
- Kutokwa na usaha ukeni
- Kutokwa na damu isiyo ya hedhi
- Maumivu wakati wa kujamiiana
- Kutokwa na damu ukeni kwa wanawake waliokwisha koma hedhi

JE, NI TABIA ZIPI HATARISHI ZINAZOWEZA KUPELEKEA MWANAMKE KUPATA UGONJWA HUU WA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI?

- Kuanza ngono mapema katika umri mdogo (chini ya miaka 18)
- Uvutaji wa sigara au tumbaku
- Kuwa na wapenzi wengi, au kujamiiana na mtu mwenye wapenzi wengi
- Kuzaa idadi kubwa ya watoto hasa wanawake walioanza kuzaa wakiwa na umri mdogo (chini ya miaka 18)

UTAGUNDUAJE MAPEMA KAMA UNA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI

Kwa kufanyiwa uchunguzi wa mdomo wa kizazi kwa wataalamu wa afya angalau mara 1 kwa mwaka.



MATIBABU

Matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi hutolewa kulingana na hatua za ugonjwa na hali ya mgonjwa. Huduma za matibabu hutolewa kwa kutumia njia zifuatazo:

- Upasuaji katika hatua za mwanzo za ugonjwa
- Mionzi
- Dawa za saratani
- Mionzi pamoja na dawa za saratani

NIFANYE NINI ILI KUPUNGUZA/KUEPUKANA NA UWEZEKANO WA KUPATA SARATANI YA MDOMO WA KIZAZI?

- Kupata chanjo dhidi ya kirusi cha Human Papilloma Virus (HPV)
- Kuepuka ngono katika umri mdogo, chini ya miaka 18
- Kuwa na mwenzi mmoja mwaminifu
- Kutumia kondomu wakati wa kujamiiana
- Kuepuka uvutaji wa sigara na tumbaku
- Kufanyiwa uchunguzi wa saratani ya mdomo wa kizazi angalau mara 1 kwa mwaka
- Kuwahi mapema kwa uchunguzi na matibabu punde tu upatapo dalili.

